

Shukrani

Kwanza kabisa ningependa kutoa shukrani za dhati kwa Prof. Mohamed Rajab, Mkuu wa Chuo Kikuu cha Pwani, kwa kujitolea kwa hali, mali na wakati katika shughuli za jarida hili na kuhudhuria mikutano hapa Pwani na RISSEA ili kuhakikisha kwamba muungano huu wa Chuo Kikuu cha Pwani na RISSEA umefanikiwa pamoja na mradi wetu wa kwanza wa kutoa jarida la Kiswahili. Zaidi ya hayo, Prof. Mohamed Rajab ameahidi kufadhili mradi huu wa jarida kwa miaka mingine mitano hadi uwe na msingi thabiti wa kuweza kujisimamia wenyewe. Tunamuomba Mwenyezi Mungu (S.W.T) amuneemeshe Prof. Mohamed Rajab neema kubwa kubwa.

Pili shukurani zimwendee Bw. Kassim Omar, Naibu Mkurugenzi wa RISSEA, kwa kujitolea kwa hali na mali pia na kufuatilizia mambo ya ushirikiano kati ya RISSEA na Chuo Kikuu cha Pwani. Shime PU! Shime RISSEA! Shukrani nyingi pia ziendee jopo la wahariri; Prof. Rocha Chimera, Prof. Beja Karisa, Dr. Nancy Ngowa, Bw. Mohammed Karama, Bw. Khalid Kitito, Dr. Rukiya Harith na Bw. Ali Wasi Mwabaya, kwa bidii na ushirikiano wao katika kuhakikisha kwamba shughuli hii yote ilienda vyema.

Pongezi pia kwa mwanamitambo ya tarakilishi katika Chuo Kikuu cha Pwani Bw. Henry Amunga kwa usanii wake wa mchoro mwafaka wa jalada la jarida hili.

Waandishi wa makala mbalimbali katika jarida hili pia hawawezi kusahaulika kwa jinsi ambavyo walijitokeza hima walipoulizwa waleta makala yao. Kwa kweli jarida hili ni fahari kwa wasomi na wapenzi wa lugha ya Kiswahili, si kwa Kenya pekee bali ulimwengu mzima.

Prof. Beja S. Karisa

(Hivi sasa ni marehemu)

Mkuu wa Shule ya Sanaa na Sayansi za jamii

Chuo Kikuu cha Pwani

BURIANI

Profesa Stephen Karisa Beja

*Imeandikwa na
Prof. Rocha Chimera
(Pwani University)*

Ni miaka miwili tangu Zirail- yule malaika wa mauti alipotupokonya mwenza Profesa Steven Beja Karisa. Ijumaa Tarehe 20.11.2015 ni tarehe ambayo inakumbukwa kwa majonzi makuu kwa familia yake pamoja na wenza wake hapa Chuo Kikuu cha Pwani.

Prof. S. K. Beja alikuwa na mchango mkuu katika uanzilishi wa jarida hili. Alifanya juhudi zote kuhakikisha kwamba jarida hili limesonga mbele katika matayarisho ya uchapishaji wake. Hata hivyo, hakuishi kuona toleo la kwanza la jarida hili. Tunamkumbuka na kumpa heshima kwa bidii aliyofanya katika kazi hii. Mwenyezi Mungu amweke mahali pema peponi.

